Shirika la Kazi Duniani
Mpango wa Kimataifa unaohusu UKIMWI na Ulimwengu wa Kazi

## Ujumbe kutoka kwa Juan Somavia, Mkurugenzi-mkuu wa ILO

Ninayo furaha kupata fursa ya kuwasilisha mwongozo wa ILO kuhusu UKIMWI na Ulimwengu wa Kazi kwa washiriki wetu wakuu wote na wale wote wanaojishughulisha katika jitihada za kupambana na UKIMWI .

Mlipuko wa UKIMWI ni janga kubwa katika ulimwengu mzima, linalotoa changamoto nzito ya kuzuia maendeleo ya kijamii na kiuchumi. UKIMWI huyaharibu maisha ya watu binafsi, ya familia zao na jumuiya; unayahusu makundi yote katika jamii, wazee na vijana. Katika nchi zilizoathirika zaidi, UKIMWI umeharibu maendeleo yaliyochukua miaka mingi kupatikana. UKIMWI ni tishio halisi linalohatarisha maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

UKIMWI ni tatizo la kijamii na kikazi kama ambavyo ni tatizo la kiafya. Unaathiri ulimwengu wa kazi kwa namna mbalimbali: huathiri sana watu ambao ni nguvu kazi za uzalishaji na hivyo kupunguza kiasi cha mapato yanayotarajiwa; huongeza gharama za matumizi kwa mashirika ya sekta zote kwa sababu ya kupungua kiasi cha uzalishaji, kuongezeka kwa gharama ya nguvu kazi, na kupoteza watu wenye ujuzi na uzoefu wa kazi.

UKIMWI unaathiri upatikanaji wa kazi na unaweza kupunguza uwezo wa watu na nchi kufanya kazi na kutoa ajira.

UKIMWI unaathiri lengo la msingi la ILO la kuwafanya wanawake na wanaume kupata kazi zenye heshima na zenye kipato kizuri katika mazingira ya usawa, uhuru, ulinzi, na hadhi. UKIMWI moja kwa moja unahusu masuala ya kanuni na haki za msingi katika kazi. Ubaguzi katika sehemu za kazi ni mfano mmojawapo. Hebu tafakari kuhusu athari kwa watoto katika wakati ambao kwa kiasi kikubwa ajira ya watoto inapigwa vita ulimwenguni pote, Watoto walio yatima kutokana na UKIMWI wanajikuta wakijitegemeza wenyewe na ndugu zao wa karibu, na inawezekana wakawa wanawasaidia wazee wasioweza kufanya tena kazi. Watoto kama hawa wako katika hali ya hatari kubwa ya kujishughulisha na kazi za hatari.

Wengi walioathirika kutokana na UKIMWI hawana misaada yoyote ya hifadhi ya jamii wala ya matibabu. UKIMWI hauna mipaka ya kijiografia au ya kijamii. Hata hivyo, hujitokeza zaidi pale palipo na umasikini, ukandamizaji, uhamiaji pamoja na uhalifu katika jamii. Watu masikini ndio wanaoteseka mno. Tofauti za kukosekana kwa usawa wa kijinsia zinazohusu tofauti za kijamii, kiuchumi na kiutamaduni-huwafanya wanawake kuwa katika hatari ya kirahisi zaidi hivyo swala hili liangaliwe kwa makini mno kwa kulenga masuala ya jinsia. Kimsingi, UKIMWI unadhoofisha kila eneo la usalama katika jamii.

Mwongozo huu wa utekelezaji juu ya UKIMWI na Ulimwengu wa Kazi unaonyesha dhamira ya ILO katika kuhakikisha mazingira mazuri ya kazi zenye heshima katikati ya matatizo ya kibinadamu na

maendeleo. Kwa kupitia mwongozo huu, ILO inatoa msaada kwa watekelezaji wengine wa kimataifa na kitaifa katika kulinda haki na hadhi ya wafanyakazi na watu wote walioathirika. Mwongozo unazingatia zaidi mahali pa kazi kwa sababu wengi kati ya walioambukizwa na kuathirika ni wafanyakazi. Ni matokeo ya ushirikiano kati ya ILO na sehemu zake tatu, pamoja na washiriki wa kimataifa, haswa UNAIDS. Mwongozo huu utakuwa ni chombo cha kusaidia kudhibiti kuenea kwa mlipuko huo, kupunguza athari zake kwa wafanyakazi na familia zao, na kutoa mafao ili kuwawezesha kukabiliana nao.

Mwongozo unatoa kanuni za msingi zinazopaswa kufuatwa na serikali, vyama vya wafanyakazi na waajiri, na wadau wengine wanaohusika. Umelenga katika kuziheshimu haki za msingi za wafanyakazi na unazungumzia yafuatayo:

- kinga kwa kutoa habari, elimu, programu zinazohusu maswala ya kutambua masuala ya jinsia, na kusaidia watu kubadili tabia;

- kulinda haki za wafanyakazi, pamoja na ulinzi wa ajira zao, usawa wa kijinsia, stahili ya kupata mafao, na kutobagua kwa sababu ya mtu kuwa na UKIMWI;

- kujali an kutoa msaada, pamoja na upimaji na utoaji wa ushauri nasaha kwa hiari na kwa siri, pia kutoa matibabu katika sehemu zile ambazo huduma za afya ya jamii hazitoshelezi.

Mwongozo wa ILO wa utekelezaji wa UKIMWI na ulimwengu wa kazi ni chombo kiongozi katika kukabiliana na matatizo ya sasa katika jamii na kutathmini athari za siku za usoni za mlipuko huo na athari zake katika ulimwengu wa kazi. Lakini mwongozo huu ni mwanzo tu, kinachohitajika zaidi ni utekelezaji wake.

Ninawasihi ninyi nyote kuufanya mwongozo huu kuwa wenu.Unaweza kuboreshwa na kutumika katika kukabiliana na mahitaji mbalimbali katika hali tofauti. Utategemea sana uhamasishaji wa serikali, waajiri na wafanyakazi kwa ajili ya utekelezaji mzuri.